SHULE YA SEKONDARI KIRUGU,
S.L.P 232,
KIGOMA.
Barua pepe mwanaishadinani@gmail.com
Simu No. 0766871748/0620699354

Kumb No KRGS/3988/2020/10
JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………….
S.L.P………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDA KIRUGU WILAYA YA KIGOMA UJIJI MKOA WA KIGOMA MWAKA 2020**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 Shule ya Sekondari Kirugu ipo umbali wa kilomita tano (5Km) upande wa mashariki kutoka yalipo makao makuu ya Halmashauri Ya Manispaa Kigoma Ujiji.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwakuripoti shuleni kuanzia tarehe 01/01/2021 mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 saa nane kamili mchana.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE YA SHULE

#### WAVULANA

a) Shati nyeupe mbili mikono mifupi sio za kubana mwili
b) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivo na na muundo wa buti za jeshi
c) Soksi ndefu nyeusi na si nyinginezo
d) Suruali mbili za rangi nyeusi zenye mifuko mitatu, Linda 2na pindo chini iwe ya kuachia mwili siyo modo zingatia sana hii.
e) Sare ya michezo T-shirt ya blue, viatu vya raba na bukta nyekundu kwa ajili ya michezo
f) Sweta rangi ya blue

#### 2.1.2 WASICHANA.

a) Shati nyeupe mbili za mikono mirefu kwa wanao vaa hijabu na kitambaa cheupekichwani na shati 2 nyeupe mikono mifupi kwa wasio vaa hijabu Viatu vyeusi vya ngozi na kisigino kirefu

Scanned with CamScanner

b) Juba lifunike viganja vya mikono ikiwa ameachia mikono chini
c) Soksi ndefu nyeupe
d) Sketi mbili, rangi nyeusi ndefu za kufunika miguu ziwe za marinda yasiozidi sita na kitambaa kiwe kigumu na siyo cha sukari.
e) Viatu vyeusi vya kamba sio raba wala bajaji
f) Raba kwaajili ya michezo
g) Sweta la bluu
h) Sketi nyekundu, tisheti ya bluu na raba kwa ajili ya michezo

**NB: kwa wote wasichana na wavulana waje na picha 4 za paspoti stemp size**

## 2.2 MAHITAJI MUHIMU.

- Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu na begi la madaftari na si Rambo wala aina nyingine ya mabegi mfano yenye urembo.

## 2.3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.1 ya mwaka 1995. aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni ( preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare za shule wakati wote.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.

## 3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Uulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine,mirungi, kubeli n.k

Scanned with CamScanner

e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mamba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mamba
k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi.

## 3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medical Examination form ijazwe na kurudishwa shuleni katika hopitali ya serikali tuu.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

....................................

**MWANAISHA ADINANI NGAYERA**
**MKUU WA SHULE**

HEAD OF SCHOOL
KIRUGU SECONDAP
P.O. BOX 232
KIGOMA

Scanned with CamScanner